

# TANDALE CHAKULA BORA

## WATER FOR AFRICAN CITIES

UN HABITAT
FOR A BETTER URBAN FUTURE

1

# UTANGULIZI

Tandale chakulabora ni makazi ya kipato cha chini yaliyoko katika kata ya Tandale katika mji wa Dar es Salaam. Makazi yapo katika kitongoji cha makazi mengine maarufu yasiyopangwa ya Manzese, yaliyo na wakazi wengi, ukosefu wa huduma za kijamii za kuaminika kama vile maji, usafi wa mazingirana na milipuko ya magonjwa. Hali ya kijamii na kiuchumi ya eneo hilo linapingana na maana ya jina lake ambalo lina maanisha ***"Chakula Bora"***



Wanafunzi wanafaidi upatikanaji wa maji masafi. **© UN-Habitat**

Idadi ya watu wa kata ya Tandale inakadiriwa kuongezeka hadi 69,999 ambayo 31,099 itakuwa ya wanaume na wanawake 38,900. Jamii ina kaya 19,537. Msongamano wa Tandale ni zaidi ya 450/km$^2$.

Kulingana na takwimu za sensa ya taifa iliyofanyika mwaka 2000 idadi ya watu wa kata ya Tandale inakadiriwa kuongezeka hadi 69,999 ambayo 31,099 itakuwa ya wanaume na wanawake 38,900. Jamii ina kaya 19,537. Msongamano wa Tandale ni zaidi ya 450/km2. Jamii ina shule ya sekondari inayokadiriwa kuwa na wanafunzi na waalimu wapatao 1,600 ambao wanajumuishwa katika idadi ya watu wa Chakula Bora.

Kulingana na utafiti uliofanywa na Mshauri aliyeajiriwa na DAWASA pamoja na UN-Habitat kubainisha mahitaji ya mafunzo kwa shule na jamii inayoizunguka, huduma ya uhakika ya usambazaji wa maji ilipewa kipaumbele cha kwanza kuliko huduma nyingine za msingi. Licha ya ukweli kwamba eneo hili limefikiwa na mtandao wa usambazaji wa maji safi wa Dar es Salaam, wakazi wa eneo hili wameendelea kukosa huduma ya maji kwa sababu mahitaji ya maji katika jiji la Dar es Salaam yanazidi kiwango halisi cha maji yanayosambazwa kwa sasa.

Kwa misingi hiyo, DAWASA kwa kupitia kitengo chake maalumu cha Mawasiliano na Jamii kiliandaa mpango utakaojitegemea wa kutoa huduma ya maji kwa shule na jamii ambao utahusisha kisima kirefu, tanki



Kukuza usafi shuleni kwa kutumia vituo vya kunawia mikono. **© UN-Habitat**



Mkutano wa mashauriano na wanawake juu ya mahitaji ya maji na usafi. **© UN-Habitat**

la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 5000 na vituo vya kushote maji ili kupunguza makali ya ukosefu wa maji. Mradi haukuwa na matawi katika jamii inayoizunguka shule na wala haukuwa na kipengele cha usafi wa mazingira. Mfumo huo ulileta migogoro mingi ya ki-uendeshaji na ki-usimamizi ambayo ilipelekea mradi kufa mwaka 2001. Baada ya hapo hapakuwa na juhudi zozote za makusudi za kuufufua mradi na kurudisha huduma kwa jamii ambayo ilikuwa inahitaji huduma.

Kwasababu hiyo jamii ya Tandale Chakula Bora iliathiriwa vibaya ki ustawi wa jamii - kiuchumi na pia kufanya mazingira ya kujifunza ya wanafunzi wa Manzese Shule ya Sekondari ambayo ni sehemu ya jamii kuwa magumu. Hali ilihitaji jitihada za wakati kushughulikia zinahitajika matatizo yaliyokuwepo. Hivyo DAWASA na UN-Habitat kwa pamoja waliungana na kutengeneza na kutekeleza mradi uliolenga kushughulikia matatizo yaliyokuwepo kupitia ukarabati wa miundombinu iliyopo, ugani wa huduma ya maji kwa jamii za jirani na kuongeza kipengele cha usafi wa mazingira katika mradi.

DAWASA na UN-Habitat walisaini mkataba wa makubaliano ya kufufua uendeshaji wa mradi kwa kufanya matengenezo makubwa ya miundo mbinu ya mradi pamoja na kuunda muundo wa kitaasisi ambao utasimamia na kuhakikisha kuwa mradi unaendeshwa kwa ufanisi na kuwa endelevu.

Vipengele vyote vya mradi huu vimekamilika na kugharimu kiasi cha dola za kimarekani 110,000. Kijitabu hiki kinakupatia mchakato mzima wa utekelezaji wa mradi na pia kitakuwa na manufaa kwa watu fani mbalimbali na pia kitatumika kwa ajili ya afua baadaye.

2

# MRADI

Mradi wa Ugani wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Tandale Chakula Bora ulitekelezwa na DAWASA na UN-Habitat ambao ndio wadhamini wakuu. Kwa sababu ya uhalisia wake mradi wa jamii wa usamabazaji wa maji na usafi wa mazingira wa Tandale Chakula Bora ulihitaji mchakato maalum wa utekelezaji ili kuhakikisha kuwa shule pamoja na jamii wanafikiwa na kuhudumiwa kikamilifu.

## Malengo ya mradi

Lengo kuu la mradi ni kuboresha maisha ya shule ya Sekondari Manzese pamoja na jamii ya Tandale Uzuri kwa hutoaji wa huduma za uhakika, nafuu na endelevu za maji na usafi wa mazingira. Yafuatayo ni malengo maaluma ya mradi ambayo yanatokana na lengo kuu;

i. Kutoa huduma ya maji yenye uhakika, unafuu, endelevu na kuboresha haki ya usafi na usafi wa mazingira shuleni na katika jamii

ii. Kujenga uwezo wa walengwa katika kusimamia mradi pamoja na miundo mbinu yake

iii. Kuunda muundo wa kitaasisi ambao utaongeza ufanisi, uwajibikaji na uendelevu katika uendeshaji wa shughuli za kila siku za mradi

## Wigo wa mradi

Mradi umelenga watu wapatao 1,600 ukijumulisha na jamii ya shule ambao ni asilimia 25 ya watu wa kata ya Tandale, na yafuatayo yametekelezwa na mradi.

- Ukarabati wa miundo mbinu ya kusambazia maji, kisima , vituo vya kuchotea maji na nyumba ya kuinulia matanki ya maji.
- Ujenzi wa mfumo mpya wa kusambazia maji wenye urefu wa Km 4.5, matenki( lita 5,000 mpaka lita 40,000) pamoja na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji ndani na nje ya eneo la shule.
- Ujenzi wa mfumo wa mfano wa kuvunia maji ya mvua.
- Ukarabati wa vyoo vya shule na ujenzi wa miundo ya kuoshea mikono.
- Uundaji wa muundo wa kitaasisi na kutoa mafunzo ya kuijengea kamati ya uendeshaji uwezo wa kuendesha na kusimamia mradi kupitia;

> *„Ilikuwa ni usumbufu na si salama kwa wana jamii kuchota maji katika eneo la shule.*
> *Naupongeza mradi kwa mpango wake wa kuipatia jamii inayoizunguka shule maji, kwani sote lazima tuishi na kuhudumiwa kwa utaratibu.*
>
> *Mr.Linus Mwakasege . Mwl. Mkuu*

- Uhamasishaji
- Mafunzo
- Utengenezaji wa mkakati wa jamii wa kujitegemea
- Kuendesha kampeni za kuhamasisha usafi na usafi wa mazingira shuleni.


Ujenzi wa tanki la kuvuna maji ya mvua. © UN-Habitat



3

# MPANGO WA UTEKELEZAJI

## 3.1 Mchakato wa Utekelezaji mradi




## 3.2 Utambuzi wa Tatizo

Kabla ya utekelezaji wa mradi kuanza utafiti maalum ulifanyika ili kubainisha matatizo na sababu zilizopelekea kufa kwa mradi, na hali halisi ya miundo mbinu, hali ya huduma iliyopo na pia miundo ya muda na bajeti kwa ajili ya kufufua mradi

## 3.3 Makubaliano ya Fedha za Mradi

Makubaliano ya ufadhili wa mradi ulizingatia mapango wa fedha, gharama za vipengele na ufadhili / Mchango. Mpango huu ulijumuisha ujenzi (vifaa) na program ya mafunzo ya kujenga uwezo. Jumla ya bajeti iliyotengwa ilikuwa dola za kimarekani 115,000. Gharama za vipengele hii ni pamoja na utafiti wa msingi na mafunzo ya kujenga uwezo uligharimu dola za kimarekani (US$.35,000), miundo, ugavi na ujenzi (US$.80,000). UN-Habitat iligharimia asilimia 90% ya gharama zote za mradi na asilimia 10% iliyobakia iligharimiwa na DAWASA.

## 3.4 Kusainishwa kwa mkataba

Mkataba wa makubaliano kati ya DAWASA na UN-Habitat uliorodhesha na kubainisha majukumu na wajibu wa kila madau. Wakati UN-Habitat alikuwa na jukumu la udamini wa kifedha na kuratibu hatua za utekelezaji wa mradi, DAWASA walikuwa na jukumu la kuratibu na kufuatilia shughuli zote za utekelezaji wa mardi na kuwafuatilia wadau wote wa mradi

## 3.5 Uhamasishaji na Ushirikishaji wa Jamii

Ili kuwahamasisha na kujenga uwelewa kwa jamii, program za uhamasishaji zilifanyika sambamba na utoaji wa mafunzo ya kujenga uwezo. Mchakato huu ulihusisha shughuli zifuatazo:-

- Uandaaji wa mikutano ya jamii katika ngazi mbalimbali
- Maandalizi na utoaji wa program ya mafunzo
- Kuandaa semina ya wadau kwa ajili ya kupitia na kupeana uzoefu
- Kuandaa mfumo wa kitaasisi unaohusisha pande zote za jamii

Mchakato wa utekelezaji wa mradi kwa uasili ulikuwa shirikishi, na jamii zinazonufai-

*Ni vizuri kuwa mradi utaendeshwa na sisi wenyewe kupitia viongozi tuliowachagua wenyewe. Ni matumaini yangu kuwa hawatatuangusha na kuturudisha tulikotoka* *Bw. Hassan Rashid mwana jamii*

ka na mradi zilishirilikishwa kikamilifu katika zoezi zima. Hatua hiyo ilitumika ili kuhakikisha kuwa jamii nufaika zinaelewa kinagaubaga uasili na ugumu wa mradi, pia hisia za umiliki wa mradi zinajengeka katika jamii. Haya ndiyo mambo muhimu sana kwa maswala ya kujitoa na uwajibikaji na hatimaye kufanya mradi kuwa endelevu.

### 3.6 Miundo na Manunuzi

Mchakato wa kuendeleza miundo na manunuzi ya watoa huduma kwa bidhaa na huduma ulifanyika kwa kuzingatia mahitaji, viwango na taratibu zilizowekwa. Taaluma na mwenendo wa maadili ulizingatiwa kuhakikisha bidhaa zitakazozalishwa na mradi zinafikia viwango vinavyotakiwa ili kufikia malengo ya mradi.

### 3.7 Mchakato wa Ujenzi

Shughuli za ujenzi zifuatazo zilitekelezwa na mradi:-

- Ukarabati wa kisima kilichopo ndani ya eneo la shule na kujenga nyumba ya kusimamishia matenki
- Ukarabati wa miundo ya vyoo vya shule pamoja na kuweka miundo ya kuoshea mikono
- Ujenzi wa miundo mipya ya kuhifadhia maji Ujenzi wa mfumo mpya wa kusambazia maji pamoja na vizimba vitano vya kuchotea maji
- Ujenzi wa mfumo wa mfano wa kuvunia maji ya mvua shuleni
- Ujenzi wa jengo jipya ya stoo



Nyumba mpya iliyojengwa ya kuhifadhi maji na vifaa. **© UN-Habitat**

### 3.8 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mradi

DAWASA na UN-Habitat wameendelea kufuatilia na kutathimimni hatua za utekelezaji wa mradi na kutoa ripoti. Baada ya mradi kukamilika DAWASA itaendelea kufanya usimamizi wa uendeshaji wa mradi kuhakikisha unaendeshwa kwa ufanisi na kuwa endelevu.

4

# MAISHA BAADA YA MRADI

Kama ilivyosemwa hapo mwanzo, shule imekuwa ikiendeshwa bila maji wala vyoo vyenye heshima na usafi ambavyo vingefanya mazingira ya kujifunza na kufundishia kuwa mazuri. Asha Ally mwanafunzi wa kidato cha tatu ana haya ya kusema kuhusiana na uzoefu wake wa hali kabla na baada ya mradi.



Asha Ally - mwanafunzi

"Ukosefu wa maji na miundo bora ya choo shuleni uliniiathiri katika mambo makuu mawili. Kwanza uliathiri uwezo wangu na wanafunzi wengine wa kujifunza tulipoteza muda mwingi kutafuta maji kwa matumizi mbalimbali ya shule na zaidi nilipotaka kwenda chooni. Pili kwa sababu ya kunywa maji machafu na tabia zisizo za kisafi nilikuwa nikisumbuliwa mara kwa mara na magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji machafu hasa kuhara. Hebu fikiri msichana wa rika langu kwenda chooni bila maji? Hiyo ilikuwa mbaya siyo kwangu tu bali hata kwa wanafunzi wengine na hata na waalimu maana hata wao walikuwa wanapata shida hiyo. Sasa maji yanapatikana shuleni hatusumbuki tena kutafuta maji na natumia vyoo kwa amani, na pia sasa ninatumia njia sahihi za usafi na kama msichana utu wangu umerudishwa"

*Shuhuda hizo mbili zinakazia umuhimu wa mradi katika kuboresha maisha ya shule na wakazi wa Tandale Uzuri kijamii na kiuchumi.*



*Wanajamii wakichota maji katika kioski nje ya eneo la shule*

Hivyo hivyo katika jamii ya Tandale hali ya upatikanaji wa maji ni ya shida ingawa mtandao wa maji safi wa Dar es Salaam upo lakini huduma zake si za uhakika. Bi Rehema Kobelo mkazi wa Tandale Chakula Bora ana haya ya kusema kuhusiana na mabadiliko yatakayoletwa na mradi huu wa maji.



"Mradi huu utatupunguzia wanawake adha ya kutembea mwendo mrefu na kupanga foleni kwa muda mrefu kupata maji na pia gharama za manunuzi ya maji zitapungua kutoka Shs. 4000 hadi Sh. 2000 kwa siku. Na afya za watu zitahimarika na hatutakuwa na manung'uniko na mabomba makavu kwa sababu sasa tuna maji kutoka katika kisima chetu cha jamii. Nawashukuru wote waliohusika katika kutuletea mradi huu"



Maji kwa wote. © UN-Habitat/Julius Mwelu

# 5

# KILICHOFANYIKA (HARDWARE & SOFTWARE)



Ujenzi wa tanki la kuvuna maji ya mvua. **© UN-Habitat**

| S/N | Item | Unit | Quantity |
|---|---|---|---|
| 1 | Matanki ya kuhifadhia maji | liters | 40,000 |
| 2 | Minara ya matenki ya urefu wa mita 3 & 6 | No | 2 |
| 3 | Mtandao wa usambazaji wa maji | Km | 4.5 |
| 4 | Vituo vya kuchotea maji | No | 5 |
| 5 | Ukarabati wa matundu ya vyoo vya shule | No | 24 |
| 6 | Mfumo wa mafano wa kuvunia maji ya mvua | No | 1 |
| 7 | Kisima kirefu chenye mita 75m na kuzalisha 8.8m3/h | No | 1 |
| 8 | Mnara wa kuinulia matenki | No | 1 |
| 9 | Miundo ya kuoshea mikono | No | 8 |

*Jedwali 5.1 miundo mbinu iliyokarabatiwa na mradi*

Kwa kutimiza malengo ya mradi, inafaa kusema kuwa mradi umefanikiwa katika malengo na matakwa ya watekelezaji na walengwa. Jedwali 5.1 hapo chini linaonyesha idadi ya miundo mbinu iliyojengwa ama kukarabatiwa na mradi.

Kwa mujibu wa jamii husika matokeo ya mradi huu yamekwenda zaidi ya uboreshaji wa miundo mbinu. Yafuatayo ni matokeo yasiyo ya moja kwa moja ambayo yametokana na utekelezaji wa mradi:

- Muundo bora wa usimamizi wa kitaasisi
- Jamii imejengewa uwezo na ufahamu kupitia mikutano, mafunzo na midahalo
- Upatikanaji wa maji yenye uhakika ambayo yatahimarisha afya za wananchi
- Imeboresha huduma ya vyoo vya shule
- Nafuu kubwa ya bei ya maji kulinganisha na bei ya wachuuzi
- Kwa ujumla mazingira na hali ya kujifunza imeboreka

Wanafunzi wapata maji salama safi ya kunywa. © UN-Habitat



6

# MASOMO WALIOJIFUNZA DAWASA

Utekelezaji wa mradi wa maji wa Tandale Chakula Bora si tu umeweza kuboresha ustawi wa jamii wa shule na jamii inayoizunguka, lakini pia DAWASA imeweza kujifunza katika nyanja kuu mbili kama zilivyoelezewa na Bi. Neli Msuya mkuu wa kitengo cha mahusiano ya jamii



Ukarabati wa vyoo shuleni unaendelea. **© UN-Habitat**

- Mitaala ya kufundishia usimamizi na uendeshaji wa miradi iliyotengenezwa na mradi, imethibitika kuwa na ufanisi wa hali ya juu katika kusimamia na kuepusha migogoro kwa miradi ambayo inasimamiwa kwa pamoja baina ya shule na jamii.

- Mpangilio wa kitaasisi uliopo Tandale Chakula Bora chini ya makubaliano ya uendeshaji, ndio muundo bora kwa miradi ya jamii inayohitaji usimamizi wa pamoja. Ikizingatiwa kuwa mradi huu ulikuwa umesimama kwa zaidi ya miaka saba kutokana na migogoro ya usimamizi kati ya uongozi wa shule na jamii. DAWASA iko katika mchakato wa kuiga mfumo huu kwenye miradi yake yote ya jamii inayohitaji usimamizi wa pamoja, ikianzia na mradi wake wa maji wa shule na jamii unaoendelea Kipunguni B.

- Utekelezaji wa mradi wa Tandale Chakula Bora ulikuja na wazo la kuzalisha kipato cha ziada kama mkakati wa kujisaidia. DAWASA imepongeza sana wazo hilo na imedhamiria kuutumia mfumo huu katika utekelezaji wa miradi yake yote ya maji ya jamii. Mbali ya kuboresha kipato cha familia za jamii nufaika, mfumo huu utaleta mapato mbadala mbali na mapato yatokanayo na mauzo na huduma za maji. Kulingana na uzoefu wa DAWASA moja ya vikwazo vikubwa katika kuendeleza miradi ya maji ya jamii ni mgawanyo wa fedha za mradi kwa ajili ya shughuli nyingine za jamii mbali na lengo la utekelezaji na huduma la uendeshaji na usimamizi wa mradi (O&M). Hii inasababishwa na ukweli kwamba jamii hazina vyanzo mbadala vya mapato kuhudumia shughuli zingine za jamii na hivyo kutegemea mapato ya mradi pekee.

Tanzania yaadhimisha shughuli za mashirika ya Umoja wa Mataifa, mashirika yote kutekeleza kama shirika moja Tanzania. © UN-Habitat/Anne Musotsi



7

# MIPANGO YA BAADAYE YA MRADI

Mradi wa usambazaji wa maji na usafi wa mazingira wa Tandale Chakula Bora umekamilika. Lakini jamii zilizo pembezoni mwa eneo la mradi hazina huduma ya uhakika ya usambazaji wa maji safi hii imesababisha mahitaji kuongezeka kuzidi uwezo wa mradi kuhudumia jamii zote husika. Hii ni changamoto ambayo inahitaji ufumbuzi kutoka walengwa wa mradi pamoja na watekelezaji wa mradi. Kwa sababu hiyo DAWASA imebainisha mpango kazi ambao utaendelea kutekelezwa na utahusisha mambo yafuatayo:

- Kusaidia jamii kupanga na kutekeleza mpango wa huduma ya gharama nafuu na upanuzi wa mradi kuyafikia maeneo / jamii ambazo hazikufikiwa na mradi.
- Kutoa mafunzo kwa jamii husika kupitia kamati ya muundo wa kitaasisi
- Kutoa ushauri wa kiufundi katika masuala ya ufundi, uendeshaji na udhibiti wa fedha za mradi.
- Kuendesha kampeni za usafi na usafi wa mazingira kwa jamii husika pamoja na shule
- Kutathimini matokeo ya mradi kwa kuzingatia malengo ya mradi
- Kusimamia uendeshaji wa mradi kupitia ripoti mbalimbali

### Programu ya UN- Habitat ya maji kwa miji ya Afrika

Malengo na mkakati ya maendeleo ya milleniam kuhusu upatikanaji wa maji ni kupunguza nusu ya idadi ya watu wasiokuwa na idadi ya maji endelevu na salama ifikako mwaka 2015.

Mkutano wa Dunia wa mwaka 2002 wa maendeleo endelevu (WSSD) uliongeza lengo lingine linalosema kuwa ifkapo 2015, idadi ya watu ambao hawna huduma ya vyoo.

UN-Habitat imechangia katika kufikia malengo haya ya Milleniamu kwa kubuni program ya maji na usafi wa mazingira wenye vipengele mbalimbali kufikia mabara mengine hususani katika nchi zinazoendelea. Moja ya vipengele hivyo ni mpango wa maji katika miji ya Afrika maarufu kama WAC. Mpango wa maji katika miji ya Afrika unalenga kuchangia mafanikio ya maji na usafi wa mazingira yanayohusiana na malengo ya milleniumu na mkutano wa dunia juu ya malengo endelevu kwa kushiriki na kuboresha usimamizi na utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira hususani katika makazi yasiyokuwa rasmi katika miji ya Afrika.
Awamu ya kwanza ya mpango huu ilikamilika kwa mafanikio mwaka 2003, na awamu ya pili inatekelezwa katika miji 17 katika nchi 14 barani Afrika.

Lengo kuu la program hii ni kushughulikia tatizo la maji na usafi wa mazingira kwa kusimamia kwa ufanisi mahitaji ya maji, kujenga uwezo na kupunguza athari kwa mazingira ya kimji juu ya rasilimali za maji baridi na kuongeza uelewa na kubadilishana taarifa juu ya usimamizi wa maji na mbinu za uhifadhi. Lengo hili lina vipengele sita vya thematika

- Kufuatilia uwekezaji na utawala
- Kuboresha usafi kwa maskini wa mjini
- Usimamizi wa msangazi mijini
- Usimamizi wa mahitaji mjini
- Elimu ya maji mashuleni na kwenye jamii
- Utetezi, kuongeza uelewa, kubadilishana mawazo
- Kuingiza maswala ya jinsia katika maji na usafi wa mazingira
- Mafunzo ya kujenga uwezo



Upatikanaji wa maji hufanya mazingira ya shuleni yawe safi na mazuri ya kujifunzia. **© UN-Habitat**

## Mipango ya Dawasa katika kuhudumia maskini wa Mijini

Dawasa ni mamlaka iliyo huru inayotoa huduma ya maji safi na maji taka katika jiji la Dar-es-Salaam, mji mdogo wa Kibaha na Bagaoyo na vijiji vilivyo kando kando ya mitandao yake mikubwa miwili.

Kama miji mingine mikubwa katika Afrika, DAWASA imekuwa ikikabiliwa na changamoto zinazofanana katika mwendo wa kufanya majukumu yake makubwa ambayo kwa asilimia kubwa, hususan katika maeneo ambayo hayako katika mtandao wake wa huduma.Kwa bahati mbaya maeneo haya hutoa makazi kwa idadi kubwa ya watu, na wengi wao ni wa kipato cha chini. Ni wazi ukosefu wahuduma ya maji ya kuaminika husababisha wakazi wa maeneo haya kuambukizwa magonjwa ya milipuko yanayotokana na maji.

Ili kukabiliana na changamoto hizo DAWASA kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali imechukua hatua kadhaa kwa lengo la kuboresha maisha ya jamii hizo kwa kutoa huduma ya kuaminika, rahisi na endelevu ya maji na usafi wa mazingira (WSSP) ili kuongeza uwajibikaji. DAWASA imeanzisha kitengo ari cha mahusiano na jamii ambacho kinahusika moja kwa moja na jamii za kipato cha chini.

Baadhi ya mipango ya DAWASA ni pamoja na:-

- Utekelezaji wa mpango wa maisha ya mstari wa ushuru
- Utekelezaji wa mfuko wa mpango mpya wa maunganisho ya kwanza
- Utekelezaji wa program ya usambaji wa maji na usafi wa mazingira kwa jamii

Kwa kupitia kitengo hichi, DAWASA imeanzisha, kutekeleza na kusimamia zaidi ya miradi 250 ya maji inayojitegemea.



www.unhabitat.org

PICHA YA JEDWALI LA MBELE
Wanafunzi wananawa mikono wakati wa muda wa mapumziko shuleni Arusha, Tanzania. © **UN-Habitat/Julius Mwelu**

PICHA YA JEDWALI LA NYUMA:
Maji safi na salama. © **UN-Habitat**

**UN-HABITAT:**
Tekalign Tsige Sahilu, Regional T. Advisor (Anglophone)
Water for African Cities Programme,
Urban Basic Services Branch
P.O.Box 30030, GPO Nairobi 00100, Kenya
T: +254 (20) 762 5166  M: +254 724 797 185
E: Tekalign.Tsige@unhabitat.org

**DAWASA:**
Neli Msuya, Community Liaison Manager
Dar Es Salaam Water and Sewerage Authority (DAWASA)
Dunga/Malanga Street, Mwananyamala
P.O.Box 1573 Dar Es Salaam, Tanzania
T: +255 2227 60015  M: +255 784 266 660
E: msuyan@gmail.com

UN-HABITAT